United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA

FEBRUARI 2007 n° 5
ISSN 2071-7784





## Maafikiano 2003

KUIDHINISHWA NA MATAIFA KUFIKIA JANUARI 18, 2007

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMANI
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 UHABESHI
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 JAMHURI YA MOLDOVA
42 YORDANI
43 SLOVAKIA
44 UBELGIJI
45 UTURUKI
46 BUKINI
47 ALBANIA
48 ZAMBIA
49 ARMENIA
50 ZIMBABWE
51 CAMBODIA
52 JAMHURI YA YUGOSLAV YA MAKEDONIA YA AWALI
53 MOROCCO
54 UFARANSA
55 CÔTE D'IVOIRE
56 BURKINA FASO
57 TUNISIA
58 HONDURAS
59 SAO TOME AND PRINCIPE
60 ARGENTINA
61 UFILIPINO
62 BURUNDI
63 PARAGUAY
64 JAMHURI YA DOMINICA
65 GUATEMALA
66 HISPANIA
67 KYRGYZSTAN
68 MAURITANIA
69 UGIRIKI
70 LEBANON
71 NORWAY
72 AZERBAIJAN
73 URUGUAY

# Mnamo Novemba 2006, Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama ilikutana Algiers ikafanya mkutano wake wa kwanza

Mnamo Novemba 18 2006, Bw. Koichiro Matsuura ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, alifungua rasmi mkutano wa Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama mjini Algiers. Bw. Matsuura alitoa shukrani zake kwa wenyeji wa Algiers kwa sababu ya ukarimu wao pamoja na mchango wao mkubwa waliotoa ili kufanikisha mkutano huo. Kadhalika, alimshukuru Bw. Bedjaoui ambaye ni Waziri wa Mashauri ya nchi za Kigeni wa Algeria, pamoja na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu. Katika hotuba yake ya makaribisho, Bw. Bedjaoui alifafanua turathi za tamaduni zisizogusika kama "thamani kubwa inayochangia katika kujenga upya ubinadamu halisi katika ufalme usio na wakimbizi kwa manufaa ya wote".

Katika hotuba yake ya makaribisho, Mhe. Bi. Khalida Toumi ambaye ni Waziri wa Utamaduni nchini Algeria, alisisitiza kwamba Turathi za Tamaduni Zisizogusika "kila mara ni kazi inayoendelea, inayokua, kuongezeka na kuundika", akahitimisha kwamba "turathi zisizogusika ni kitambulisho cha watu ilhali ramani ya DNA ni ya nasaba ya binadamu". Wanakamati wote 24 wa Mataifa Wanachama walishiriki;Mataifa 16, Mataifa Wanachama 20, Mataifa yasiyo Wanachama na Mashirika 3 yasiyokuwa ya serikali yalikubaliwa kushiriki kama watazamaji. Bi. Toumi alichaguliwa kama Mwenyekiti kupitia ukubalifu wa wote. (yaendelea uk. 2)



© CNRPAH 2004

*Washiriki katika mkutano wa kwanza wa Kamati ya Turathi Zisizogusika mjini Algiers walitumbuizwa na kikundi cha waimbaji waitwao Ahellil ambao ni watumbuizaji wa ngoma ya kienyeji kutoka Gourara. Ngoma hii ilitangazwa kama Kito cha Masimulizi katika mwaka wa 2005.*

## Tahariri

Mwaka wa 2006 umekuwa mwaka wa mavuno. Wafanyi kazi wa kitengo cha Turathi Zisizogusika wameongezwa na kuhamishiwa orofa ya tisa ya jengo la UNESCO liitwalo Bonvin. Kituo kipya cha habari na wavuti wa Maafikiano vinafanya kazi. Kadhalika, kitengo cha Turathi Zisizogusika kilisaidia kutayarisha mipango ya utendaji kuhusu Vito vya thamani ishirini vilivyotangazwa mwaka wa 2005 huku kikisimamia miradi endelevu inayohusisha Vito vya thamani vya 2001 na 2003. Katika mwaka huu wa shughuli nyingi kitengo cha Turathi Zisizogusika kilishirikiana pia na wengine katika kutayarisha au kushiriki kwenye mikutano mingi ya serikali za nchi, au hata ile ya wataalamu ulimwenguni.

Tukio lingine muhimu katika mwaka wa 2006 lilihusisha ufunguzi wa Peru ya CRESPIAL huko Cuzco, kituo cha kwanza katika kategoria 11 ambacho ni kituo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika kilichoundwa ili kuendeleza kazi za Turathi za Tamaduni Zisizogusika katika Latini Amerika. Vituo vingine vinatayarishwa katika Jamhuri ya Korea na Algeria.

Katika harakati hizi, kitengo cha Turathi Zisizogusika kilijitwika jukumu muhimu kama kituo cha Maafikiano. Pia huu ulikuwa mwaka wa kihistoria uliosubiriwa kwa hamu ili kuyapata Maafikiano hayo kisheria. Baada ya Maafikiano kukubaliwa kutumika mnamo Aprili 2006, Kikao Kikuu cha UNESCO kilifanya mkutano wa kawaida (Juni) na usio wa kawaida (Novemba), kisha Kamati ya serikali za nchi ilikutana Algeria katika mkutano wake wa kwanza mwezi wa Novemba.

Vyombo vyote viwili sasa vina afisi na sheria za utendakazi ambazo zinaviwezesha kuanza kufanya kazi. Kufikia mwishoni mwa mwaka, zaidi ya Mataifa Wanachama 70 yalikuwa yameidhinisha Maafikiano. Toleo hili la *Messenger* linawasilisha muhtasari wa mikutano hiyo miwili iliyobainishwa hapo juu. Habari zaidi zinapatikana katika wavuti wetu.

Katika mwaka wa 2007, toleo la *Messenger* litaendelea kukutaarifu kuhusu shughuli muhimu za Turathi za Tamaduni Zisizogusika, ikiwemo ile mikutano miwili ya Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama iliyopangwa pamoja na shughuli zingine zinazotayarishwa. Kwa wasomaji wetu wote wanaochangia katika lengo letu la kuhakikisha kunawiri kwa turathi za ulimwengu, tunatuma salamu za heri za mwaka wa 2007 wenye mafanikio.

*Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*

*Uchina ambayo itakuwa mwenyeji wa Kikao cha kwanza kisicho cha kawaida cha Kamati ya serikali za nchi. Uchina imekuwa mshirika mkubwa katika miradi ya UNESCO ya Turathi Zisizogusika kama ilivyoshuhudiwa kupitia kutangazwa kwa aina tatu za Vito vya thamani vya kitaifa, pamoja na Kito cha Masimulizi kimoja cha kimataifa kiitwacho Urtiin Duu, yaani wimbo mrefu wa Mongolia na Uchina. Uyghur Mugam ya Xinjiang ilitangazwa kuwa Kito cha thamani kwenye mwaka wa 2005 na kutambuliwa kama kipengele muhimu cha turathi za maisha yao ambapo Uyghur ni mojawapo ya jamii ndogo zaidi nchini Uchina.*



© Liang Li

## Kikao cha kwanza kisichokuwa cha kawaida cha Mkutano Mkuu

Kulingana na Mkataba, uanachama wa Kamati ya serikali za nchi ulihitaji kuongezwa kutoka wanachama 18 hadi 24 wakati ambapo idadi ya Mataifa Wanachama itakapotimia 50. Idadi hii ilitimia kunako mwezi Agosti wakati taifa la Zimbabwe lilipokuwa mwanachama wa 50. Kutokana na hili, Mkutano Mkuu uliitisha kikao kisicho cha kawaida katika Makao Makuu ya UNESCO tarehe 9 Novemba ili kuchagua wanachama sita zaidi.

Kwanza Mkutano Mkuu ulijadili uwezekano wa kuwa na idadi mahsusi ya viti katika kila kikundi cha uchaguzi ndani ya Kamati. Kwenye mwezi wa Juni 2006, tayari Mkutano Mkuu ulikuwa umeamua kugawanya viti hivyo kwa usawa kupitia kigezo cha mtawanyiko wa kijiografia huku ikizingatiwa kuwa angalau viti vitatu vingepewa kila kikundi.

Ikiwa uzingativu huu ungetiwa maanani, kikundi cha 1 cha uchaguzi (Uropa na Marekani Kaskazini) kingalipewa viti viwili, kukiwa kumepungua kimoja katika hivyo vitatu. Tatizo hili lilitatuliwa wakati kikundi cha Afrika kilipotoa kwa ukarimu na kwa njia ya kipekee kiti kwa kikundi cha 1. Mkutano Mkuu uliamua kuahirisha mjadala kuhusu idadi ya mwisho ya ugavi wa viti hivyo hadi kwenye kikao kijacho. Baada ya hapo, wanachama wapya wa Kamati wapatao sita walichaguliwa: Belarus, Bolivia, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ufaransa, Mali na Syria. Kutokana na hili, Mkutano Mkuu ulichagua wanakamati 12 kwa kupiga kura (wawili kutoka kila kundi) ambapo muda wao wa utendakazi ni miaka miwili. Mpango huu unauwezesha Mkutano Mkuu kuchagua upya nusu ya wanachama wa Kamati katika kila mwaka wa pili, kuanzia 2008.

**WANACHAMA 24 WA KAMATI NA MASHARTI YAO YA UTENDEKAZI**

| KUNDI I | | KUNDI IV | |
|---|---|---|---|
| UBELGILJI | 2006 - 2008 | UCHINA | 2006 - 2008 |
| UFARANSA | 2006 - 2008 | HINDI | 2006 - 2010 |
| UTURUKI | 2006 - 2010 | UJAPANI | 2006 - 2008 |
| **KUNDI II** | | VIET NAM | 2006 - 2010 |
| BELARUS | 2006 - 2010 | **KUNDI V (a)** | |
| BULGARIA | 2006 - 2008 | JAMHURI YA AFRIKA YA KATI | 2006 - 2010 |
| ESTONIA | 2006 - 2010 | GABON | 2006 - 2010 |
| HUNGARY | 2006 - 2010 | MALI | 2006 - 2010 |
| ROMANIA | 2006 - 2008 | NIGERIA | 2006 - 2008 |
| **KUNDI III** | | SENEGAL | 2006 - 2008 |
| BOLIVIA | 2006 - 2008 | **KUNDI V (b)** | |
| BRAZIL | 2006 - 2008 | ALGERIA | 2006 - 2008 |
| MEXICO | 2006 - 2010 | JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA | 2006 - 2008 |
| PERU | 2006 - 2010 | UMOJA WA MILKI ZA KIARABU | 2006 - 2010 |

## Kikao cha kwanza cha Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama (yaendelea toka uk.1)

### Masharti ya utendakazi yaliyoundwa na Kamati

Swala la kwanza la Kamati lilihusu utendakazi. Mambo mawili muhimu yalichochea mazungumzo. 'Je, ni vipi **swala la uwakilishi wa kijiografia** litaheshimiwa katika harakati zote, likiwemo swala la uchaguzi wa Mataifa Wanachama kwa zamu ambao Kamati inahimiza?'

Wanachama wa Kamati walikubaliana kwamba Ofisi ya Kamati pamoja na matawi yake yote yaimarishwe kulingana na maswala hayo. Aidha, walikubaliana kwamba Maafikiano yanaipa Kamati mamlaka kuteua kwa muda matawi yoyote ambayo yataona ni muhimu ili kutekeleza kazi yake. Sheria zitakazozingatiwa ili kuanzisha mamlaka hayo zilizua mjadala mkubwa, huku baadhi ya Mataifa Wanachama yakisisitiza kuwepo kwa matawi kama hayo kwa muda. Yalieleza kwamba yangeiruhusu Kamati kushughulikia bila masharti mahitaji yoyote ya matawi hayo ambayo yataweza kujitokeza.

Baadhi ya wanachama pia walipendekeza kwamba sera ilihitaji matumizi ya lugha zote sita za utendakazi katika Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, wengine walitaja kwamba uwekevu ulihitaji matumizi ya lugha mbili za utendakazi, huku wakieleza kwamba pesa zinazohitajika kutafsiri na kufasiri lugha zingine nne zaidi hazitapatikana hasa pia kuwawezesha wawakilishi kutoka katika Mataifa Wanachama yanayoendelea. Kufanya hivyo pia hakutawezesha utekelezaji wa kazi za uhifadhi wa turathi. Hivyo, Kamati ilihitimisha kwamba lugha mbili za utendakazi ziwe Kiingereza na Kifaransa, lakini pia pesa zitafutwe kwa namna zozote zile ili lugha zingine pia ziweze kutumika.

### Maongozi ya Utendakazi

Rasimu iliyotayarishwa kwa muhtasari iliwekwa mbele ya Kamati ili iweze kutoa mwongozo kwa Afisi ya Utendakazi hasa katika utayarishaji wa rasimu za nyaraka mbalimbali ambazo baadaye zitahusishwa kwenye maongozi hayo.

Mapendekezo mbalimbali yaliungwa mkono: Mojawapo ni kutafuta maana za istilahi zilizoko katika nyaraka zote ili kukuza uelewa wao kuhusu turathi za tamaduni zisizogusika, eneo ambalo bado ni geni katika sehemu nyingi. Baadhi ya wanachama walielezea matumaini yao kwamba umma, mataifa na jamii mbalimbali zinazojali zitaona umuhimu wa kuimarisha hatua za kulinda turathi, mbali na kusisitiza kuwepo kwa uzingativu, uelewa, utambuzi na uwazi katika kufanya hivyo.



© Liang Li



© Liang Li

## Vigezo vya rasimu ya uandishi wa Vito vya Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwenye Orodha ya Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kibinadamu

Wanachama walikubaliana kwamba vigezo hivyo viwe rahisi kubadilishwa ili viweze kushirikisha turathi za tamaduni zisizogusika mbalimbali zilizoko ulimwenguni. Kadhalika, walisisitiza kwamba vigezo hivyo vinatarajiwa kubadilika kulingana na ongezeko la tajriba na dhana zinazoibuliwa kulingana na wakati. Ijapokuwa hali ya Orodha ya Turathi za Ulimwengu iliweza kutoa vitangulizi muhimu, wanachama walikubaliana kwamba Orodha hiyo awali ilitokana na kichocheo tofauti, kulinda turathi-hai.

Maoni tofauti yalitolewa kuhusu uhusika wa jamii za watu katika kutoa kibali cha kuandikwa kwa masimulizi au hata desturi zao kwenye Orodha. Wanachama wengine walisaili jinsi kibali kilicho "huru ambacho kilitolewa awali na ambacho kinatokana na ufahamu" wa jamii husika kinavyoweza kurekodiwa kikamilifu katika hali ambapo kuna wingi wa miundo tofauti ya kisheria katika Mataifa Wanachama. Wengine walipendekeza kwamba kuwepo kwa kito cha turathi katika jamii fulani kwa miongo au hata milenia ni ithibati tosha ya kuiwezesha jamii hiyo inayokitekeleza kutoa kibali. Wanachama wengine walionyesha kutoridhika kwao kuhusu jamii kutoa kibali, mbali na kurekodiwa.

Hata hivyo, wanachama wengine walisisitiza kwamba kigezo cha kuihusisha jamii kinatokana na lugha yenyewe ya Maafikiano, na kwamba Kamati haina mamlaka ya kuondoa masharti yake. Wengine walibainisha kwamba kutokana na tajriba za nchi zao, turathi zilizoimarishwa kwa kushirikiana na jamii husika zilifaulu lakini zile zilizoimarishwa bila kuhusisha jamii hazikufaulu. Mwishowe, baadhi ya wanachama walipendekeza kwamba vigezo vya ulinzi huo lazima vizingatie kuhusisha jamii badala ya kuimarisha kanuni zinazolenga kukubali kwao; ikiwa zilihusishwa kikamilifu katika hatua zote basi hiyo ni ishara kubwa ya kukubali kwao.

### Jopo la utendakazi la Kikao cha kwanza cha Kamati

- Mhe. Bi. Khalida Toumi wa Algeria, Mwenyekiti
- Bw. Jean-Pierre Ducastelle wa Ubelgiji, Mwandishi wa mkutano
- Bolivia, Uchina, Estonia na Senegal, Manaibu Wenyeviti.

## Uwezekano wa kurekodi Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwenye Orodha Wakilishi kwa kipindi fulani

Wanachama wengine waliunga mkono wazo kwamba vito vya Turathi za Tamaduni Zisizogusika vingeondolewa kutoka katika Orodha baada ya muda fulani ili kuvipa nafasi vingine. Waliona kwamba hii ni njia muafaka ya kutoa nafasi kwa vito vya kitamaduni vingi zaidi kujulikana kimataifa na kupata sifa huku urefu wa Orodha hiyo ukiweza kuhimiliwa. Wengine waliona kuwepo kwa mageuzi katika Orodha hiyo kunaenda sambamba na asili ya turathi zisizogusika kwani kila wakati hizi ziko katika kujiunda upya na kujitanua zenyewe. Hata hivyo, wanachama wengine walitoa maoni yao kwamba kurekodiwa kwa kito cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwa muda mahsusi kunaweza kuchukuliwa kama kitu duni ikilinganishwa na kule kukaa kwa muda mrefu kwenye Orodha ya Turathi za Ulimwengu. Wanachama kadha walihofia kwamba muda wa kito kuwa katika Orodha utakapoisha, inaweza kuchukuliwa kama dharau au kudunisha jamii na taifa husika, hata kama hili silo kusudio.

Wanachama wengi walipendekeza kwamba uhifadhi kwa kawaida huchukua muda mrefu, na kwamba muda wa kito kukaa katika Orodha unaweza kuisha kabla hata ya kuweza kuhifadhiwa ipasavyo. Pendekezo moja lililotolewa ni kwamba kito kinaweza kurekodiwa tena au pia kwamba muda wa kukihifadhi hauhitaji kukadiriwa kwa kuzingatia muda wa kurekodiwa. Ili kubainisha taswira mbalimbali pamoja na kuweza kutumia utaalamu ulioko katika Mataifa Wanachama, Hindi ilipendekeza kwamba ingetayarisha mkutano wa wataalamu katika miezi ya karibuni nchini humo. Kamati iliamua kuyapa moyo Mataifa Wanachama kupitia kwa njia ya kutuma maombi na mapendekezo yao kwa Afisi Kuu. Aidha, ilimwomba Mkurugenzi Mkuu kuiwasilishia vigezo vilivyotayarishwa upya ili vijadiliwe katika Kikao kinachofuata.



© Liang Li

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752

MHARIRI MKUU Rieks Smeets

JOPO LA UHARIRI Fernando Brugman, Richard Lo Giudice, Frank Poschan, Reiko Yoshida

MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

*Toleo la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika* linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania.

Nakala ya Kiarabu imewezeshwa kupitia kwa mchango wa kifedha wa Mamlaka ya Utamaduni na Turathi ya Abu Dhabi, Milki ya Abu Dhabi – U.A.E.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika (www.unesco.org/culture/ich) na kupigwa chapa bila malipo ilimradi mwandishi atambuliwe.


© Conselho das Aldeias Wajãpi-Apina

# turathi zisizogusika

## KALENDA

**FEBRUARI 9-10** Mkutano wa Wataalamu: "Kutambua Desturi Nzuri katika Kuhifadhi Lugha Zinazohatarishwa Afrika Kando ya Jangwa la Sahara" Addia Ababa, Uhabeshi.

**FEBRUARI 21-23** Mkutano wa Wataalamu: UNESCO – ACCU "Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika kupitia kwa Elimu Rasmi na Isiyo Rasmi" Chiba, Ujapani.

**MACHI 14-16** Mkutano: Turathi Zinazogusika na Zisizogusika: "Mikutano Miwili ya UNESCO" Montreal, Canada.

**APRILI 2-4** Mkutano wa Wataalamu kuhusu "Orodha za Maafikiano ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika na Vigezo vya kuzichagua" New Delhi, Hindi.

**APRILI 12** Kuzindua Maonyesho ya Picha: "Turathi-Hai: Kuchunguza Zisizogusika" UNESCO Fontenoy, Paris.

**MEI 23-27** Kikao cha Kwanza kisicho cha kawaida kinachohusisha Kamati ya serikali za nchi kuhusu Uhifadhi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Uchina.

**SEPTEMBA 3-7** Kikao cha pili cha kawaida kinachohusu Kamati ya serikali za nchi kuhusu Uhifadhi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Ujapani.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na: ich@unesco.org

## KAMATI MAALUM YA SERIKALI ZA MATAIFA WANACHAMA (inaendelea)

### Usaidizi wa Ushauri– majadiliano yataendelea

Maafikiano yanaiamuru Kamati kupendekeza kwa Mkutano Mkuu vigezo na vielelezo vitakavyotumiwa *kuyatambua rasmi mashirika yasiyo ya serikali ambayo yana umahiri katika mawanda ya turathi za tamaduni zisizogusika ili yawe washauri*. Kamati ilikubali kwamba Maafikiano ya 2003 yalihitaji mfanyiko jumuishi wa mashauriano lakini haikuweza kuamua ni muundo gani mfanyiko huo utachukua au jinsi mashirika mengi yasiyokuwa ya serikali yatakavyoweza kuhusishwa kikamilifu katika kazi ya Kamati hiyo.

Wanachama wengine waliunga mkono uwezekano wa kuwa na tawi moja kuu ambalo lingeratibu mawasiliano baina ya Kamati na mashirika mengi yasiyokuwa ya sserikali. Wanachama kadha walisisitiza umuhimu wa kuzingatia kuwepo kwa uwakilishi wa kijiografia miongoni mwa mashirika hayo. Baadhi ya wanachama walipendekeza pia kwamba wasizingatie tu yale mashirika yasiyokuwa ya serikali bali pia wahusishe wajuzi na zile jamii mbalimbali ambazo huenda zisitambuliwe kama mashirika yasiyokuwa ya serikali au kuwakilishwa na mashirika hayo. Kwa hakika, wanachama walikubaliana kwamba nafasi kubwa haina budi kukita katika lugha ya uamuzi wa Kamati kuhusu jambo hili, na uamuzi huo lazima uzingatie wataalamu na vituo vya kitaalamu. Kamati iliamua kujadili jambo hili zaidi huku ikiyaomba Mataifa Wanachama kutoa maoni yao kwa Afisi ya Utawala. Aidha, ilimwomba Mkurugenzi Mkuu kukusanya maoni hayo kuwa kama pendekezo ambalo litazingatiwa katika kikao kijacho.

### Hatua inayofuata – mikutano iliyopangwa kufanywa Uchina na Ujapani

Kamati ya serikali za nchi ilitoa maamuzi kuhusu tarehe na mahali pa mikutano ijayo. Serikali ya Uchina iliialika Kamati hii kufanya kikao kisichokuwa cha kawaida kuanzia tarehe 23 hadi 27 Mei 2007 nchini Uchina. Serikali ya Ujapani nayo ilitoa mwaliko wa kufanywa kikao cha pili nchini humo mwanzoni mwa mwezi wa Septemba 2007. Mialiko hii ilipokewa kwa moyo mkunjufu na Kamati.

Tawi jipya rasmi lilichaguliwa na Kamati kuhudumu mpaka mwisho wa kikao cha Ujapani:

- Mhe. Bw.Seiichi Kondo wa Ujapani kama Mwenyekiti
- Mhe. Ousman Blondin wa Senegal kama mwandishi wa mkutano
- Ubelgiji, Bolivia, Estonia na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria kama Manaibu Wenyeviti.

(Kikao kisichokuwa cha kawaida kitachagua tawi lake rasmi.)


© Umemura Yutaka


© Umemura Yutaka

*Jumba la Maonyesho la Kabuki lilitangazwa kuwa Kito cha Thamani mwaka wa 2005. Aina ya uigizaji wa kiasili Ujapani uitwao Kabuki huwasilisha kazi muhimu za fasihi ya kirasimi huku ikisawiri matukio ya kihistoria na upinzani katika mahusiano ya kimaadili. Uimbaji, mandhari ya kuvutia, wahusika wa kiume waliovaa maleba na mapambo ya kuvutia huku wakicheza kwa miondoko mahsusi huchangiana ili kuifas*